# JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

# MONITORING LEARNER'S PROGRESS

## GREDI YA NANE – 004

## KISWAHILI LUGHA – KARATASI YA 2

Jina ________________________________________

Jinsia Mvulana ☐ Msichana ☐

Jina la Shule ________________________________________

1. **Kuandika – Alama 15**

**Insha yako iwe na kati ya maneno 300-350.**

**Mwandikie rafiki yako barua ya kirafiki huku ukimweleza mbinu au njia mbalimbali zinazoweza kutumika kudumisha usafi katika sehemu za umma.**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

1. **Fasihi simulizi-'alama 10**

Kiangazi kilikuwa kimesambaa kila eneo. Wanyama walikuwa wamemaliza akiba yao yote ya maji. Kisima kimoja tu ndicho kilichosalia na maji. Kulingana na chura aliyekilinda, kisima hicho kingeweza kutoa maji kibuyu kimoja tu baada ya siku mbili.ilibidi wanyama waandae kikao ili kuamua namna ya kuyatumia maji hayo yaliyokuwa yameadimika kama mizizi ya mawe.

Mfalme wao simba alieleza kuwa wote wangeangamia wasingechukua tahadhari. "Ndugu zangu, lazima tupange namna ya kutumia bidhaa hii adimu na kila mmoja aipate kwa usawa.

Baada ya mkutano wa muda mrefu, wanyama wote waliamua kwa kauli moja kukilinda kisima chao. Hayo yote yalipokuwa yakiendelea, sungura alionekana kuzama katika lindi la mawazo. Usiku huo sungura alipitisha mfereji chini chin ya ardhi na kuunganisha kibuyu chake na kisima. Hata hivyo sungura hakujua kuwa mahali mfereji ulipitia kulikuwa makao ya Fuko.

"Itawabidi wanyama kuniletea chakula ndipo wapate maji kwangu", Sungura alijisemea. Maji yalikosekana kisimani kwa siku saba. Mlinzi akalaumiwa. Walinzi kadhaa wakabadilishwa bila mafanikio. Kila wakati maji yalitoweka. Fuko alipeleka ujumbe kwa simba kuwa alimwona sungura akipitisha mfereji chini ya ardhi. Sungura alipofikishwa kwa hakimu wao mfalme simba, aliomba msamaha kuwa hangewanyima tena wenzao haki zao.

a) Hadithi hii ni ya aina gani? Eleza. **Alama 2**

______________________________

b) Bainisha mandhari yanayojitokeza katika dondoo hii. **alama 1**

______________________________

c) Taja changamoto kuu iliyowakumba wahusika katika dondoo hii. **alama 2**

______________________________

d) Andika sifa tatu za aina ya hadithi uliyoitambua katika swali la (a). **alama 3**

i) ______________________________

ii) ______________________________

iii) ______________________________

e) Eleza funzo moja kuu linalojitokeza katika hadithi hii. **alama 2**

______________________________________________________________

2. **Novela – alama 10**

Mama Siti alikuwa mjane mwenye watoto watatu. Aliuza maandazi mjini kila uchao ili kukidhi mahitaji ya wanawe. Maisha yalikuwa magumu lakini hakukata tamaa. Kila siku aliomba Baraka kwa kazi yake. Alikuwa na ndoto ya kuwaona watoto wake wakiishi maisha mema zaidi kuliko alivyopitia yeye. Ingawa hali ilikuwa ngumu, Mama Siti alijua fika kuwa jitihada huwa na thamani na kwa Imani aliona ipo siku mambo yangebadilika.

Siku moja alipokuwa sokoni, alikutana na mwanamume mmoja aliyemnunulia maandazi mengi. Mwanamume huyo alikuwa mgeni mjini na alionekana mwenye huruma. Alimwambia mama Siti alikuwa mwekezaji na alitaka kusaidia kina mama waliojitegemea. Mama Siti aliguswa na msaada wa ghafla na alijua kuwa fursa hii ingeweza kubadili maisha yake nay a watoto wake. Baada ya wiki moja, mama Siti aliitwa kwenye mkutano wa kina mama wajasiriamali. Aliteuliwa kuwa katibu wa chama kipya cha akina mama wajasiriamali. Walianzisha mpango wa kupeana mikopo midogo kwa biashara ndogondogo.

Kupitia chama hicho, maisha ya mama Siti yalibadilika. Aliweza kufungua duka dogo la vyakula na kuwalipia watoto wake karo. Kijiji kilianza kumtambua kama kiongozi mwenye moyo wa kusaidia. Mama Siti aliona nafasi ya kubadilisha jamii nzima, si tu maisha yake. Aliandaa semina za kuwasaidia wanawake wajasiriamali wengine na kuwafundisha umuhimu wa kupanga bajeti na kuweka akiba. Hali ya kijiji ilianza kubadilika, wanawake walikuwa na uweza wa kujitegemea na familia zao zilikuwa na matumaini mapya.

a) Bainisha mandhari katika sehemu hii ya novela. **Alama 1**

______________________________________________________________

b) Bainisha wahusika watatu kutoka katika kifungu hiki. **Alama 3**

i) ______________________ ii) ______________________

iii) ______________________

c) Mama Siti alikuwa na changamoto ipi kama inavyojitokeza katika dondoo hii. **alama 1**

______________________________________________________________

d) Ni shughuli ipi iliyotajwa kuleta mabadiliko katika jamii inayozungumziwa kwenye dondoo. **Alama 1**

______________________________________________________________

e) Andika msuko wa dondoo hii. **alama 4**

______________________________________________________________

3. **Tamthlia ( alama 10)**

***Ni alasiri baada ya kushinda shambani ambapo Bi Sikitu na mumewe wameketi kwenye nyasi chini ya mti)***

**Bw Heshima:** Akionekana mwenye uchovu mwingi. Naomba angaa gilasi moja ya maji nikonge roho.

**Bi Sikitu:** Haya yataisha ni kwa muda tu mume wangu. Hatuna budi kupinda migongo yetu kwa ajili ya watoto wetu. (Akiondoka *kuingia jikoni*)

**Bw Heshima:** (*Baada ya kupiga mafunda kadhaa*) Huu ni ukweli usiopingika. Siku hizi si kama enzi zetu ambapo watoto wa kike walibaki jikoni wakipika.

**Bi Sikitu:** (*Kwa masikitiko*) Mimi mwenyewe sikuona lango la darasa la nane. Tuwekeze kwa wanawetu tukijua kuwa akiba haiozi.

**Bw Heshima:** Hili zao letu litakuwa la Fanaka. Takima sasa yuko kipindi cha lala salama katika uzamifu. Naye Bella anaendelea kujikakamua. Hii si bure. (*Akiamka mahali alikuwa na kuingia chumbani*)

**Bella:** (*Akiwa amebeba mkoba*) shikamoo mama.

**Bi Sikitu:** Marahaba mwanangu. Shuleni kwema?

**Bella:** Abe mama. Leo tulipewa matokeo ya mtihani wetu. (*Akimkabidhi matokeo*)

**Bi Sikitu:** (*Akitabasamu*) Hongera mwanangu. Matokeo mazuri haya naona hata masomo yaliyokuwa yakikulemea wakati huu umeyashinda. Nenda sasa uuweke mkoba kisha umalize shughuli zako. Mimi hapa nataka niingie jikoni niandae chajio. (*Anaingia jikoni*)

a) Bainisha mandhari katika onyesho hili. **Alama 1**

_______________________________________________

b) Huku ukitoa mifano mwafaka taja mbinu mbili ambazo mwandishi ametumia katika sehemu hii ya tamthilia. **Alama 4**

i) _______________________________________________

ii) _______________________________________________

c) Taja masuala yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo hii. **Alama 2**

i) _______________________________________________

ii) _______________________________________________

d) Eleza alivyomaanisha Bwana Heshima aliposema kuwa **"Takima sasa yuko katika kipindi cha lala salama." Alama 2**

_______________________________________________

e) Taja sifa moja ya tamthilia inayojitokeza katika dondoo hii. **Alama 1**

_______________________________________________

**4. Ushairi – alama 5**

Alinijuza mamangu, niwe mwenye tahadhari
Niwachunge walimwengu, nisifikwe na hatari.

Nilipokuwa nyumbani, walinijia wageni
Wakabisha mlangoni, nikajibu karibuni.

Ndani walipoingia, walinifunga kitini
Haraka wakanyakua, vitu vyetu vya thamani

Walipokuwa langoni, wakitaka kuondoka
Wakafika majirani, wahuni wakatoroka

Jamani tuwe makini, daima tusizembee
Tusiache asilani, usalama ulegee.

a) Shairi ni la aina gani? Eleza **alama 2**

_______________________________________________

b) Bainisha wahusika wowote wawili katika shairi hili. **Alama 2**

_______________________________________________

c) Dhamira ya shairi hili ni ipi? **Alama 1**

_______________________________________________